# *Eliya Na Sadaka Ya Unga*

Lo, hiyo si ni kweli! “Bwana, napokea.” Kupokea nini? Kila ahadi aliyotoa, ni yangu.

2 Sasa, kabla hatujaketi, hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi ili nisije nikasahau kuomba juu ya leso hizi hapa.

3 Bwana wetu, tunakushukuru Wewe usiku wa leo kwa nyimbo za Sayuni, kwa Injili ya mtindo wa kale inayosafisha mioyo yetu na maovu, na, kwani, ahadi zenye neema zaidi katika Biblia ni zetu. Kwa imani tunazipokea. Na tunajua kwamba Mungu hana upendeleo wa mtu. Na katika kizazi ambacho Paulo aliishi, watu. . . wengi sana walikuwa wagonjwa. Wakamletea leso, nguo, ili aziweke mwilini mwake, na kisha kuchukuliwa kutoka kwa mwili wake kwenda kwa wagonjwa na wanaoteseka. Na maandiko yanatuambia kwamba pepo wachafu walitoka kwa watu na mateso yakawaacha kwa sababu ya imani yao katika Bwana Yesu. Mungu, Paulo ameondoka kwa karibu miaka elfu mbili, akaja Uweponi Mwako. Kizazi hicho kilipita pamoja naye, lakini Wewe ni Mungu wa kila kizazi. Sasa watu, usiku wa leo, wamekuamini Wewe na tunakabidhi Kwako, usiku wa leo, hizi leso na vifurushi vidogo vya bidhaa, na kuamini kwa moyo wetu wote kwamba Wewe utajibu maombi yetu nao watapona. Tujalie, Bwana. Tunazituma kwao kwa utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu, Mwanawe. Amina.

4 Mnaweza kuketi. Na wale walioziweka hizi hapa wanaweza kuja kuzichukua mara tu baada ya kufungwa kwa ibada hii.

5 Nina furaha sana usiku wa leo. Nimekuwa upande mwingine wa mlima huko leo mara tu nilipomaliza mahojiano ambayo ilibidi niwe nayo, na nikaenda huko kusali. Na kila wakati ninapoingia kwenye jua hili la jangwani kwa namna fulani hunifanya nitake kurudi zaidi. Lakini jambo moja ambalo ninafurahia usiku wa leo, mke wangu. . . kadri ambavyo tumekuwa pamoja, na ameona maono makubwa ya Mungu yakidhihirishwa na kutimia. Alikuwa chini mtoni siku hiyo huko Jeffersonville wakati Malaika wa Bwana alipotokea kwa mara ya kwanza, ilisambazwa na Associated Press kote nchini. Imekuwa. . . ilikuwa 1933. Alikuwa amesimama pale, lakini aliisikia Sauti bali hakuiona Nuru. Ambapo, hata wapiga picha wa magazeti waliona Nuru. Lakini alikuwa mchanga sana wakati huo, na kama miaka kumi na miwili, naye hakuona Nuru. Alikuwa akiwatazama watu, wengi walikuwa wakizimia. Na ilibaki pale tu kwa dakika moja hivi kisha ikarudi moja kwa moja angani tena. Na magazeti yakaweka makala nzuri, “Nuru ya ajabu inaonekana juu—juu ya mhudumu wa kawaida wa

Baptisti wakati akibatiza." Ikaenda kote hadi Canada, ikaingia kwenye vyombo vya habari vya Canada.

6 Halafu kama miaka mitatu au minne iliyopita, wakati nilipokuwa huko Phoenix mwisho, ninaamini ni Ndugu Jack Moore aliyekuwa pamoja nami, ambapo yeye kwa namna fulani . . . Mke wangu ni mwoga sana. Na kwa hivyo akamwita kwenye jukwaa, bila kutarajia, na yeye karibu azimie. Naye alikuja baada ya mimi tayari kufika kwenye jukwaa, na upako ulikuwa pale kwa ajili ya ibada ya uponyaji. Na, alisema, mara ya kwanza aliyopata kuwapo katika Uwepo huo namna hiyo. Na, usiku kabla ya jana, alimwona kwenye jukwaa, kwa mara ya kwanza yeye kuwahi kumwona, wakati Hiyo ilipokuwa hapa imesimama kwenye jukwaa. Na nilipokutana naye nje yeye . . . machozi yalikuwa machoni mwake, akasema, "Billy, kwa mara ya kwanza maishani mwangu, niliiona." Alisema, "Mimi . . . ulikuwa ukimwombea mwanamke fulani, ndipo" kasema "Niliiona Hiyo ikija tu moja kwa moja mbele yake na kusimama pale kwa muda mfupi tu, ikasogea karibu na hapo ulipokuwa. Halafu, mara tu ulipoacha kuongea, ilitoweka." Kwa hivyo ninafurahi kwa ajili ya hilo, kwamba ilikuja mbele ya macho yake. Unaona, maskini mwanamke huyo ana mengi ya kupitia, na kwa hivyo nina furaha na kufurahi kwa hilo.

7 Sasa, kesho usiku ni ibada ya uponyaji. Unajua, tumekuwa tukisema wiki hii kwamba ibada za uponyaji zitakuja Ijumaa usiku. Sasa, njoo kesho alasiri au—au mapema jioni, kama saa kumi na mbili, kusudi usichachawize ibada iliyobaki. Na Billy, Leo, Gene na hao, watakuwa hapa na kadi za maombi, kukupa kadi ya maombi. Hapo ndipo tunapowaleta watu kwenye jukwaa na kuwaombea. Sasa sisi ni . . . mimi . . . Sina budi kuendesha mikutano ya Marekani kwa njia ambayo watu wamefundishwa, kuwekewa mikono. Sasa, hayo ni—hayo ni Maandiko, lakini hiyo ni mila ya Kiyahudi. Hiyo si kwa ajili ya watu wa Mataifa, lakini watu wa Mataifa huendelea nayo. Mtu wa Mataifa alikuwa, "Sistahili hata Wewe uje chini ya paa langu, sema tu Neno na mtumishi wangu ataishi." Hiyo ni kweli. Lakini Myahudi, "Njoo uweke mikono Yako juu ya binti yangu naye ataishi." Unaona, hiyo ilikuwa desturi yao, haikuwa kwa ajili ya watu wa Mataifa.

8 Usiku baada ya usiku, na saa baada ya saa, kupitia mchana na usiku, Roho Mtakatifu huja, kufunua, kupitia kwenye jengo, kuzungumza siri za mioyo. Unaiona wakati wote. Hiyo ni kukufanya ujue kwamba Uwepo wa Bwana upo hapa. Sasa, kama ungeikubali tu, ungeponywa mara moja. Maana uponyaji wote uliowahi kufanywa kwako, tayari umekamilika, umekuwa kwa miaka elfu moja mia tisa. Wokovu wote ambao utapata kupokea, tayari umelipiwa, ni yako tu kuupokea. Imekuwa miaka elfu moja mia tisa, au zaidi, tangu ilipokuwa wokovu kwako. Lakini sasa unaniona kwenye mikutano, nasema, "Je, itakufanya uamini?" Tazama, ishara na maajabu sio ya uponyaji

au wokovu, lakini ni kuwaacha watu watambue na kuelewa kwamba Uwepo wa Mungu upo hapa. Kisha Yeye. . .ikiwa Yeye. . .Jinsi ingekuwa, zaidi sana ni muujiza. Kwa urahisi tu sasa tunaanza kuona miujiza.

9 Sasa linapokuja suala la mtu, kumekuwa na watu kadhaa kati yao wameinuka kutoka kwa machela na viti vya magurudumu na kadhalika, na kutoka nje. Hiyo siyo muujiza haswa. Hapana. Unaona, hata Sayansi ya Kikristo ina hiyo. Inaweza kuwa ha—ha—hali ya akili ambayo ungeweza kuwa . . . badilisha njia yako ya kuwaza. Sasa, hatuamini ilikuwa, kwa sababu ninaamini ilikuwa imani. Lakini bado . . .

10 Nilikuwa huko La Salle, Lorraine, Ufaransa. Nilikuwa huko Paris. Nami nikashuka hadi mahali ambapo walikuwa na mwanamke aliyekufa amelala hapo, alizikwa. Nao wakasugua jiwe hapo, na watu wakaingia huko pamoja na vilema, magongo, na kuyaweka chini na kuondoka, kutokana na kusugua ule mwamba juu ya yule mwanamke aliyekufa. Unaona, amekufa, na hakuweza tena kufanya maombezi zaidi ya . . . Kuna mpatanishi mmoja tu kati ya Mungu na mwanadamu, na huyo ni Kristo Yesu. Kutoka kwenye familia ya Kikatoliki, mimi—mimi najua kwamba wanaamini katika—katika watu wanaokufa, kwamba hizo ni roho zao zinazowaombea; mbalimbali, zingine kwa siasa na zingine kwa mambo mengine. Kwangu mimi, ni ushirika na mizimu. Siumizi hisia zenu, natumai, lakini lazima niwe mkweli. Tazama, chochote kinachojipatanisha na wafu ni uabudu mizimu.

Waliniuliza huko Mexico, wakasema, “Na Yesu je?”

11 Nikasema, “Hajafa. Alifufuka tena, Yu hai hata milele.” Unaona? Hajafa, Yu hai. Hao wengine wamepita zaidi ya hayo, ambayo, Maandiko yanasema kwamba “Wale waliopo hawawezi kuja hapa, na hawa waliopo hapa hawawezi kwenda huko.” Hakuna mtu aliyewahi kuvuka au atakayewahi kuvuka. Kwa hivyo hiyo huitatua ikiwa . . . Yesu alisema hivyo.

12 Lakini tunapata vitu hivi vikifanya kazi. Kwa hivyo sasa na kila usiku Roho Mtakatifu anajaribu kukuletea Uwepo wa Utu Wake hapa, sio uwepo wa mwanadamu. Mwanadamu anaweza tu kujinyenyekeza, kwa karama anaweza kujisalimisha katika eneo fulani la Roho ambalo linaweza kukufungulia wewe Mungu. Lakini haitafanya kazi mpaka wewe mwenyewe uiamini na kuikubali, ndipo basi inafanya kazi. Tazama, ikiwa ungekaa hapo na kila mmoja wenu—kila mmoja wenu atakuwa haamini, usiamini Neno Lake, isingefanya kazi kamwe.

13 Yesu, alipokwenda kwa watu Wake mwenyewe, nchi Yake mwenyewe, matendo mengi makuu hakuweza kufanya kwa sababu ya kutokuamini kwao. Na ikiwa hakuweza kuifanya wakati huo, hawezi kuifanya sasa, kwa sababu ya kutokuamini. Unaona, ni imani yako.

14 Kwa hivyo inahitaji mimi na wewe, pamoja na Roho Mtakatifu, kufanya mambo haya yatimie; kunifanya nifurahi, kukufanya ufurahi, kwamba Mungu yuko hapa anayelitimiza Neno Lake.

15 Lakini wakati Roho Mtakatifu anapoweza kuingia kwenye mkutano, kutimiza hasa kwa Maandiko yale Yeye aliyosema yatatokea katika siku za mwisho, na kwenda juu ya wasikilizaji kama alivyofanya wakati alikuwa hapa, na kutambua siri zenyewe za mioyo, na mawazo na makusudi ya moyo na akili, mtu yeyote angewezaje kutia shaka? Unaona, huo hapo muujiza kamili, muujiza zaidi kuliko kiwete kutembea, maana haiwezekani hilo kutokea bila nguvu za kiroho. Lazima iwe ni nguvu za kiroho kufanya hivyo. Kwa hivyo, halafu unaona ni sawa tu na kile ambacho Biblia iliahidi na kile wanacho-. . . kile tunachoamini. Ni muujiza zaidi ya kupiga kelele. Tazama, ni muujiza zaidi kuliko kunena kwa lugha. Paulo alisema hivyo. Hata karama halisi za Roho Mtakatifu za kunena kwa lugha, ni muujiza zaidi ya hizo. Tuko kwenye muujiza wa mwisho. Imetabiriwa hivyo na Biblia.

16 Kwa hivyo, usiku wa leo, haikulazimu kusubiri mpaka kesho usiku kuja kupitia mstari wa kuwekewa mikono. Sasa, kukuwekea mikono hakutafanya zaidi ya kutambua mawazo ya moyo; sio sana, kwangu. Basi unaweza kuipokea tu, uishikilie, ni yako. Na unaiamini kwa moyo wako wote.

17 Lakini kesho usiku, ikiwa wewe. . .Maandiko yanasema, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkahubiri injili kwa kila kiumbe; ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Ishara zote; na kisha, mwishowe, Yeye alisema, "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hiyo ni kweli. "Wale ambao. . . " Ninii. . .Hiyo itafuatana na hao waaminio. Sawa. Sasa, sisi—sisi ni waaminio, kwa hivyo, kwa njia hiyo, tuna usiku baada ya usiku wa kuweka mikono juu ya wagonjwa, na Mungu ametenda miujiza mikubwa pamoja nao. Tumekuwa na miujiza mikubwa pamoja na kuomba juu ya leso. Tumekuwa na miujiza mikubwa na kutambua mawazo ya moyo. Tazama, yote pamoja, hufanya kazi kwa utukufu wa Mungu. Sio kwa ajili ya mwanadamu, sio kwa ajili ya kanisa, ni kwa utukufu wa Mungu. Utukufu wa Mungu!

18 Sasa, kabla ya kufungua Neno sasa kwa ajili ya usiku. . . Loo, tunaweza kugeuza kurasa *hivi,* lakini Mungu hana budi kuifungua; sababu Maandiko si tafsiri ya kibinafsi, lakini Roho Mtakatifu aliyeandika Maandiko ndiye Mfasiri wake. Basi na tuinamishe vichwa vyetu sasa wakati tukiomba. Na ni wangapi wangependa kukumbukwa katika maombi hayo, ungefanya tu ijulikane kwa kuinua mikono yako, chochote ilicho? Ee Mungu, angalia. Sisi sote tunahitaji, sivyo? Mimi ni mhitaji, pia, marafiki. Nimeinua mikono yangu.

19 Baba wa Mbinguni, kwa unyenyekevu na kwa utulivu na kwa heshima tunaingia kwenye Uwepo Wako mkuu, tukijua, kabla ya jambo hilo moja kutukia, Wewe uko hapa kwa sababu uliahidi kuwepo. Ulisema, kabla ya kuondoka Kwako, "Popote ambapo wawili au watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa hapo katikati yao. Na ikiwa watakubaliana juu ya kitu kimoja, kuhusu kitu kimoja, waombe, watapokea." Bwana, kuleta ahadi Yako kwa hili, lililonunuliwa na Damu Yako, naomba ya kwamba kila mwanamume, mwanamke, au mtoto, walioinua mikono yao usiku wa leo, Wewe unajua moyo wao, jalia wapokee kile wanachoomba. Ijalie, Bwana.

20 Sisi ni watu wahitaji. Tunatembea katika ulimwengu wenye giza, na adui wako Mkuu, ambaye, hatungeweza kupigana naye hata kidogo ikiwa haikuwa ni kwa ajili ya Roho Wako Mtakatifu. Kwa hivyo tunatumaini, tunaamini, na tunatenda kwa imani, kwamba Yeye atatutangulia na kuifanya njia iwe wazi. Mitego mingi barabarani, iliyowekwa kwa ajili ya miguu yetu iliyochoka, lakini tunajaribu kufuata nyayo za Damu za Yeye ambaye alishinda kifo, kuzimu, na kaburi.

21 Tuongoze, usiku wa leo, kwa Roho Wako Mtakatifu, Bwana, kwa Maneno yanayopaswa kusemwa, kisha uyaongoze Maneno hayo kwa moyo ambao ni mhitaji wa Hayo. Halafu, Bwana, jalia mwishoni mwa mkutano, na tukiondoka kwenda kwenye nyumba zetu mbalimbali, jalia tuweze kusema tena, kama wale waliokuja kutoka Emau, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu wakati aliposema nasi njiani?" Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

22 Kwenu mnaoandika Maandiko, geukeni pamoja nami sasa kwenye kitabu cha Wafalme wa Kwanza. Nataka kusoma fungu kutoka kwenye kifungu cha 17 . . . sura ya 17, hasa, na nitaanzia kwenye kifungu cha 14. Soma kifungu cha 14, 15 na 16 cha sura ya 17 ya Wafalme wa Kwanza:

> *Kwa kuwa* Bwana*, Mungu wa Israeli, asema hivi: Lile pipa la unga halitapunguka, wala ile chupa ya mafuta haitaisha, hata siku ile . . .* Bwana *atakapoleta mvua juu ya nchi.*
>
> *Basi akaenda, akafanya kama alivyosema Eliya; na yeye mwenyewe, na Eliya, na nyumba yake, wakala siku nyingi.*
>
> *Lile pipa la unga halikupunguka, wala ile chupa ya mafuta haikuisha, sawasawa na neno la* Bwana *alilolinena kwa kinywa cha Eliya.*

23 Hapana shaka ilikuwa karibu mapambazuko wakati alipoamshwa. Aligeuza kichwa chake kilichochoka kwenye mto aliposikia maskini kilio cha kuomboleza, kwenye chumba hicho. Na hakuwa ameweza kulala usiku kucha, alitupwa huku na huku kwa sababu ya msiba huu mkubwa. Mvulana mdogo

alikuwa ameamka tena, akiwa hajalala zaidi ya dakika ishirini au thelathini, na ninaweza kusikia sauti yake ndogo ikisema, "Mama, hivi hutatoka nje na kuangalia kabatini tena na uone ikiwa hakuna kipande kidogo cha mkate? Nina njaa sana! Siwezi kabisa kulala."

24 Na jinsi alivyoonekana katika uso wake mdogo na... mashavu yake madogo yanayozama, na macho yake madogo yakigeuka manjano, nywele zake ndefu zikining'inia kwa kukosa kukatwa, maskini shati lake la kulala lililochakaa; machozi makubwa kutoka kwa macho yake yakifoka kwenye uso wake mdogo, alipompapasa shavuni na kusema, "Mpenzi, jaribu kulala, na uelewe."

25 Kulikuwa na miaka mitatu hakukuwa na mvua juu ya nchi. Alipiga magoti sakafuni, ninaweza kumuona wakati alikuwa akimlilia Mungu, akasema, "Ee Bwana Mungu, Yehova, Wewe ndiwe Mungu wa baba zetu, Wewe uliyewalisha watoto Wako na kuwatunza kote katika miaka. Nami nimejaribu kuishi mkweli na mnyofu Kwako, na sasa nipo hapa nikimwona mtoto wangu mdogo akililia chakula, na sina kitu cha kumpa. Kwa majuma mengi sasa tumekuwa tukijinyima kufikia mahali pa kula mara moja kila siku tatu au nne, na sasa yote yamekwisha ila maskini konzi moja ya unga na kijiko kimoja tu cha mafuta. Na ninajaribu kuishikilia hadi mchana, isitokee kwamba tutakufa wakati wa usiku. Nimefanya nini, Ee Mungu? Mimi, mjakazi wako, nimeishi mkweli. Mume wangu alikufa vitani, vita kwa ajili ya Bwana, na nimekuwa mjane kwa miaka kadhaa sasa, na nimejaribu kuishi kwa njia ya haki na kushika Amri Zako. Na iwapo ni wakati wangu kwenda, sijali; lakini mvulana wangu mdogo, inaurarua tu moyo wangu vipande vipande kumsikia akiomba chakula, huku sina chochote cha kumpa."

26 Alipomaliza kuomba, aliinuka. Alikuwa amerudi kulala tena kwa dakika chache. Na alikuwa ameinua mikono yake juu, na gauni chakavu la kulalia alilokuwa amevaa lilikuwa karibu limekwisha. Anaenda dirishani na kutazama nje, na ni karibu tu mapambazuko. Loo, kulikuwa joto sana!

27 Upepo wenye joto wa hukumu ulikuwa ukivuma juu ya taifa ambalo lilikuwa limemsahau Mungu. Hiyo ilikuwa wakati wa utawala wa Ahabu, mfalme katili na mwovu kuliko wote wa Israeli. Na alikuwa ameoa mwenye dhambi, Yezebeli, ambaye alikuwa mwabudu sanamu. Na harusi iliyochanganyika kama hiyo haifanikiwi kamwe, haiwezi kabisa kuwa, ama mwanamke atakuja kwa njia ya mwanamume au mwanamume atakwenda kwa njia ya mwanamke. Naye alikuwa mwanamke mdogo mwenye kuvutia sana, na Ahabu, alikuwa tu muumini vuguvugu, alikuwa ametoa maoni yake na kusema, "Loo, vema, dini sio kitu kwangu, mimi ni mfalme." Na kwa muda mrefu walikuwa wamebomoa madhabahu za Mungu na kuweka madhabahu za Mabaali, au Baali, hasa. Na kilio kilikuwa sana dhidi ya dini

ya kweli mpaka wahudumu chini ya shinikizo kubwa walikuwa wameachilia.

28 Wakati fulani uliopita nilitoa tamshi juu ya wahudumu, au kitu kingine katika siku hii, na kikundi fulani kikakutana nami na kusema, "Ndugu Branham, makusanyiko yetu yanatuvuta tu!" Hiyo ndiyo inayosababisha hilo, kusanyiko litatoka nje ikiwa mhudumu hawafurahishi.

29 Na kwa muda mrefu wahudumu walikuwa wameanguka chini ya ushawishi wa mfalme kwa sababu dhambi iliruhusiwa, hakukuwa na mipaka. Ni picha nzuri sana ya leo kwa sababu, taifa lilikuwa limeidhinisha mambo haya, watu walitaka kuwa maarufu. Walifikiri, "Mradi taifa limesema hivyo, ilikuwa sawa." Hivyo ndivyo wanavyosema leo, "Mradi taifa linasema ni sawa kuuza bia, basi ni sawa kuinywa. Ikiwa taifa linaruhusu wanawake wetu kutembea nusu-uchi barabarani, na sheria haitawafunga, mbona, ni sawa kufanya hivyo." Hiyo inaweza kuwa sawa kwa taifa, lakini katika vitabu vikuu vya Mungu unawajibika na utalazimika kujibu mbele za Mungu. Lakini walikuwa wameanguka, ilibidi wajisalimishe chini ya mzigo huo.

30 Na taifa lilikuwa likisitawi, na walidhani kuwa ustawi ni ishara kwamba Mungu alikuwa pamoja nao. Hiyo sio ukweli wote. Mungu anakuja kwako . . .

31 Kuna methali ya zamani, methali yenye kumvunjia Mungu heshima, ambayo inasema kwamba "Mungu husaidia wale wanaojisaidia wenyewe." Hiyo ni kumkosesha Mungu heshima! Mungu husaidia wale ambao hawawezi kujisaidia. Yeye ni Mungu wa wale wanaohitaji rehema. Naye ni Mungu mwenye huruma. Na hiyo methali inayosema kwamba "Yeye huwasaidia wale wanaojisaidia wenyewe," ikiwa unaweza kujisaidia, huhitaji msaada Wake. Lakini Yeye huwasaidia wale ambao hawawezi kujisaidia wenyewe.

32 Lakini taifa lilikuwa limefikiria, maadamu walikuwa wakila vizuri na walikuwa wamevalia vizuri, kwamba kila kitu kitakuwa sawa.

33 Lakini kulikuwa na mmoja ambaye bado alikuwa wa mtindo wa kale, ambaye aliamini kwamba kuna Mungu ambaye alikuwa wa mtindo wa kale, aliamini kwamba kulikuwa na Mungu anayetimiza Neno Lake, aliamini kwamba Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo, alikuwa mtakatifu na alihitaji kujitoa kabisa kwa utakatifu Wake. Lakini Yezebeli na wafanyakazi wake mamboleo walimchukia. Alikuwa mchungaji wao, lakini hawakuamini hilo. Kwa hivyo, ilibidi ajifiche kwa ajili ya uhai wake.

34 Na Mungu alikuwa amemtuma juu mlimani, na kusema . . . mpe ujumbe, akasema, "Shuka ukamwambie maskini mfalme huyo mwovu, 'BWANA ASEMA HIVI.' Haitanyesha, au hata

umande kushuka, mpaka uuite." Akaiweka katika kinywa cha Elisha kuita mvua ilipofika wakati wake; lakini alikuwa na funguo za mbinguni, angeweza kuifunga au kuifungua. Basi Yeye akasema, "Nataka upande juu kutoka nyikani . . . ya hii . . . kuingia nyikani, hasa, kutoka kwenye machafuko haya. Toka kati yao. Umewahubiria na hawatakusikiliza wewe, na wanazidi kuwa wabaya. Nenda huko nyikani, na uketi hapo karibu na kijito, Kerithi, nami nita . . . tayari nimeamuru kunguru wakutunze." Lo, ikiwa watu hawataki, Mungu ana kunguru ambao wanaweza kufanya hivyo!

35 Yohana alisema, "Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto."

36 Yesu alisema, "Ikiwa watanyamaza, miamba itapaza sauti."

37 Mungu anaweza kufanya kile anachotaka kufanya. Alisema, "Nimewaamuru kunguru, nao watakulisha." Wakamletea nyama na mkate.

38 Mtu mmoja alisema wakati mmoja, "Waliipata wapi, Ndugu Branham?"

39 Nikasema, "Sijui. Kitu pekee ninachojua, waliileta. Waliipata kutoka sehemu ile ile ambayo Yesu alifanya alipochukua samaki watano na . . . au biskuti tano na samaki wawili, na kulisha watu elfu tano. Inatoka kwa mkono huo huo umbaji wa Mungu Mwenyezi." Wakamletea samaki na mkate, hao kunguru, wakaketi na kumkabidhi Elisha, naye akala, akainama na kunywa kutoka kwenye chemchemi. Mungu alikuwa akimpumzisha nabii Wake.

40 Loo, nina furaha sana kwamba Mungu ana njia ya kuepukia! Na wakati walidhani alikuwa mwendawazimu, "Nabii huyo mzee, maskini mkatiza-raha," kila wakati akijaribu kukatiza raha kutoka kwa maskini karamu zao za furaha walizokuwa nazo, akiwaambia kwamba ni dhambi. Na Mungu . . . yeye akifuata agizo la Mungu, akapanda milimani na kuketi juu ya mahali palipoinuka, mahali pakavu zaidi nchini. Lakini Mungu alidumisha kile kijito kikiendelea. Nao walikuwa chini huko wakitafuna ndimi zao kutafuta maji.

41 Unajua, Mungu ana njia ya kujibu maombi. Mwanamke huyu mdogo alikuwa ameishi kweli. Alikuwa hajaolewa tena, alikuwa akikaa peke yake ili kukutana na mumewe huko utukufuni. Alikuwa mwanamke mwenye heshima. Na kwa wiki pipa lilikuwa likienda chini, chini, na yeye akiendelea kuomba, na bado ilionekana kama hakuna tumaini linaloonekana mahali popote.

42 Unajua, hapo tungeweza kupata somo kutoka kwa hilo. Kwamba, ikiwa umeomba na kutimiza mahitaji yote ambayo Mungu anataka ufikie, na Yeye angali kimya, Yeye hasemi chochote, na bado umetimiza matakwa, sasa, ni nini kinachotokea basi? Ikiwa unajua kuwa umetimiza matakwa

Yake na umefanya yote unayojua kufanya, basi imani haitikisiki, inatulia tu na kuwazia mazuri. Imani huchukua msimamo wake wa kudumu kwenye Mwamba wa Miaka, nayo haitikisiki.

43 Jamaa huyo mkubwa anayeitwa "imani"! Nimesema mara nyingi, "Imani ina nywele kifuani." Wakati akiongea, kila kitu kingine kinanyamaza. Wakati imani inasema, "Nyamaza!" basi kila kitu kinasimama, kwa sababu yeye ndiye bosi.

44 Na alikuwa ametimiza kila sharti. Alikuwa ameishi safi, alikuwa ameishi kwa adabu, aliishi mwenye heshima, na alikuwa ametimiza matakwa yote ya Mungu. Lakini, ilionekana kana kwamba alikuwa kimya. Mungu hufanya hivyo wakati mwingine kukujaribu, kuona ni aina gani ya majibu utakayokuwa nayo. Usisahau!

45 Ukipita juu ya jukwaa, unaombewa, na mikono kuwekwa juu yako, na inaonekana kana kwamba hakuna kinachotokea, hiyo haisimamishi imani hata kidogo, umetimiza matakwa ya Mungu. Sasa, laiti ungeyatimiza! Sasa, ikiwa unajiepusha na Mungu, unajua moyo wako unakuhukumu . . . Nasi tunajua, "Ikiwa moyo wetu hautuhukumu, basi tunayo." Sasa, lakini ikiwa moyo wetu unatuhukumu, hakuna haja ya kuja kwenye jukwaa, hakuna haja ya kumwomba Mungu chochote, kwa sababu huna imani ya kukipokea. Lakini ikiwa umetimiza kila mahitaji ambayo Mungu anahitaji, basi imani hujitokeza hapo nje, na kusema, "Mungu ni Mungu! Nimetimiza matakwa."

46 Maandiko yanasema, "Wale wanaomngojea Bwana watafanya upya nguvu zao, watapaa juu na mabawa kama tai, watakimbia na hawatachoka, watatembea wala hawatazimia." Kama wimbo unavyosema, "Nifundishe, Bwana! Loo, nifundishe, Bwana, jinsi ya kungojea." Ioshe nafsi yangu katika Damu ya Kalvari, nitimize kila hitaji, niteketeze madaraja yote kote, na kusema, "Sasa, Bwana, sina chochote mikononi mwangu ninacholeta, kwa Msalaba Wako tu ninashikilia. Uliliahidi, Bwana." Hiyo ndiyo aina ya hali, sababu ya watu kufikiria kuwa mimi ni mtu wa kujitenga. Lakini kwenye chumba, au huko kando ya jangwa, hiyo ndiyo hali ambayo huna budi kuingia kabla ya kuja kwenye mimbara hii hapa. Kwa sababu, Shetani kila mara anaachilia vijishetani vidogovidogo kujaribu kuvuruga kitu. Na lazima uwe umeshika moja kwa moja kwenye Msalaba, bila kutegemea uwezo wako mwenyewe, mawazo yako mwenyewe, ukiegemea tu kwenye Mkono wa milele. Bila kudai akili yoyote, bila kudai akili yako mwenyewe, unajifungua tu na kumruhusu Roho Mtakatifu anene. Hiyo ndiyo hali ambayo Mungu anataka Kanisa Lake liwe. Ingia katika hali hiyo.

47 Mungu hukujaribu. Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa kwanza, aadhibiwe, ili kuona ikiwa anaweza kustahimili adhabu. Tukijitokeza na kusema, "Ninaamini

kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, kwamba alikufa kwa ajili ya dhambi zangu na akafufuka tena siku ya tatu. Alijeruhiwa kwa makosa yangu, akachubuliwa kwa maovu yangu. Adhabu ya amani yangu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake nimepona." Unaposema hivyo, pamoja na maungamo . . . dhambi zako zote na maovu yako, na uwezo wako na yote uliyo nayo, weka juu ya madhabahu. Halafu, huko, bila chochote mkononi mwako, Shetani atakurushia kila mshale awezao. Lakini basi ukigeuka kutoka hapo na kusema, "Vema, labda sikuokoka, labda sikupona," halafu ujiepushe na Hilo, Biblia ilisema wewe ni "watoto haramu, na sio watoto wa Mungu."

48 Mungu humjaribu kila mwana wa Ibrahimu kama alivyomfanya Ibrahimu, kwa kuwa sisi ni uzao wa Ibrahimu. Kwa kufa katika Kristo, sisi ni uzao wa Ibrahimu na ni warithi kulingana na ahadi. Uzao wa Ibrahimu, hiyo ndiyo roho ambayo Ibrahimu alikuwa nayo. Alikuwa na ahadi aliyopewa. Na ikiwa baba yetu alimwamini Mungu na akachukua ahadi, isiyowezekana, na kuishikilia kwa miaka ishirini na mitano kabla haijadhihirika, akipata nguvu wakati wote, uzao wake kama tu baba. Haijalishi ni nini kitatokea, tunapoombewa, imekwisha! Tukiondoa kila kitu njiani, tukatimiza mahitaji yote, na kutoa kila kitu njiani, basi mwombe Mungu, na usimame hapo ukijua utapokea.

49 Mungu alimjaribu Ayubu hivyo. Wakati Ayubu aliomba rehema, akatoa dhabihu kwa ajili ya watoto wake, kitu pekee ambacho nabii huyo alikuwa nacho ni sadaka ya kuteketezwa. Lakini hiyo ndiyo yote ambayo Mungu alihitaji.

50 Mungu hahitaji elimu na upuuzi mwingi, anahitaji moyo uliosalimishwa kwa mapenzi Yake. Hakuulizi uvae kwa njia fulani, au—au kwenda kwenye vitu fulani au kwenye vyuo fulani, au digrii. Anauliza moyo mnyenyekevu, wenye toba, uliovunjika, na ulio tayari kumpokea.

51 Alimjaribu Ayubu, na kuona ni aina gani ya majibu atakayopata ndani yake. Lakini alipochukua kondoo wake na kuchukua fahali wake, na kuchukua ngamia zake, na kuchukua watoto wake, "Nitaona Ayubu anasema nini sasa."

52 Akasema, "Bwana alitoa na Bwana ametwaa, Jina la Bwana libarikiwe."

53 Alipata kile alichokuwa amemwambia Shetani alikuwa nacho katika Ayubu, "Hakuna aliye kama yeye, duniani."

54 Kisha ngurumo zikaanza kunguruma, radi zikaanza kumulika. Roho ilikuja juu ya nabii, naye akapaza sauti, "Najua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho atasimama juu ya nchi. Ingawa mabuu ya ngozi yauharibu mwili huu, lakini katika mwili wangu nitamwona Mungu; Ambaye nitamwona mwenyewe, macho yangu yatamwona, na sio mwingine."

55 Aliwajaribu watoto wa Kiebrania ili kuona ni aina gani ya majibu wangekuwa nayo. Walikuwa wamekiri kati ya wapagani kwamba "Kulikuwa na Mungu aliye hai, kulikuwa na Yehova Mungu, na kwamba Yeye alikuwa ni Mungu wa Mbingu na Mungu wa dunia, na alishika kila nafsi mkononi Mwake." Kwa hivyo Mungu aliwaacha wajaribiwe. Na walikuwa wametimiza matakwa yote, walikuwa wameomba vya kutosha na wakaondoa kila kitu njiani. Nao hawangesujudia sanamu ya mfalme. Akaiongeza moto tanuru mara saba zaidi ya ilivyowahi kuwa. Na hapana shaka kwamba Shetani alikuwa anajaribu kuwaambia, "Huu ndio mwisho wa safari." Ninapenda jinsi walivyozungumza, "Mungu wetu anaweza kutukomboa kutoka katika tanuru hii ya moto, lakini, hata hivyo, asipofanya hivyo, hatutavunja Amri za Mungu. Tutabaki waaminifu! Acha imani yetu ipige kelele kote hata katika miaka ijayo, kwamba, tulidumu waaminifu kwa ahadi ya Mungu."

56 "Mungu wangu anaweza kuniponya kutokana na *huu*." Au, "Mungu wangu ana uwezo wa kunitoa kutoka kwenye kiti hiki cha magurudumu. Mungu wangu ana uwezo wa kufanya *hili*. Lakini nimemkubali kama Mponyaji wangu. Nimekiri dhambi zangu (kutokuamini kwangu) na kukiri kwamba ninaamini kwamba Yeye ndiye Mponyaji wangu. Ije, iende chochote kile. Ikiwa siko sawa leo, nitakuwa kesho; ikiwa siko sawa kesho, nitakuwa mwaka ujao. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, Jina la Bwana libarikiwe!"

57 Loo, hilo hapo! Na walipoingia katika tanuru ya moto, chini ya majaribio, chini ya majaribu, walibaki waaminifu hadi mwisho. Lakini Mungu alikuwepo kwa muda mfupi tu, na akawaokoa. Walijua kuwa walikuwa wameomba vya kutosha, dhambi zao ziliungamwa. Walijua walikuwa wametimiza kila hitaji, na bado Yeye alionekana kuwa kimya. Yeye yuko kimya tu kukujaribu, kuona kweli wewe ni nini, ni nini kilicho ndani yako, kuona ikiwa kweli unamaanisha kutoka moyoni mwako kile unachosema kwa midomo yako. Acha hiyo iingie kwa kilindi. Tunaweza kusema kwa midomo yetu, lakini je, moyo wetu unasema hivyo?

58 Sasa, wakati maskini mwanamke huyu alijua kwamba alikuwa ametimiza mahitaji haya yote, na bado Mungu alikuwa kimya. Ilionekana kana kwamba Yeye hakumjali hata, Yeye hakujali kama aliishi au alikufa. Lakini, wakati wote, Mungu alikuwa akifanya kazi. Hakujua juu yake, lakini Mungu alimwambia Eliya. Alikausha kijito, akanyoosha mkono Wake na kusimamisha kijito kisiteremke. Naye Eliya akasema, "Bwana, kwa nini kikasimama?"

59 Akasema, "Nimemwamuru mwanamke mjane akulishe." Alikuwa amemwamuru tayari, yeye hakujua.

60 Labda ameamuru kutoka kwako ushuhuda wa uponyaji wako; huenda usijue, lakini shikilia tu. Unapokuwa na hakika kuwa umetimiza mahitaji yote, wakati unajua kuwa umefanya kila kitu ambacho unajua kufanya, na kujiweka mwenyewe mbele za Mungu, kuna jambo moja tu la kufanya, ni, kushikilia ahadi Yake wakati huo. Kaa hapo! Mungu aliahidi kujibu, Yeye atafanya hivyo. Hujui kile Yeye alichoamuru, malaika gani, au *nini* cha kufanya. Huenda ikawa usiku huu, kabla ya ibada ya uponyaji kuanza kesho usiku. Mungu anaweza kuwa ameona hali yako leo, huenda amesikia maombi yako.

61 Niliwahurumia sana hawa watu viziwi na bubu. Ninataka kuwawekea mikono na kuwaombea, nilianza kusimama jana usiku, lakini nilisema hiyo haitakuwa sawa kwa wengine wao. Lakini ninajuaje kwamba mahali pengine si Mungu mnyamavu anayejua moyo, watu hawa wametimiza matakwa yao kwa Mungu, na wako tayari, na kuna malaika hapa usiku wa leo kuwaokoa kutoka kwa shida zao zote? Ninajuaje? Huenda Mungu ameamuru ukombozi wao usiku wa leo. Ikiwa ninawaombea wagonjwa, au sivyo, wataupata kwa sababu Mungu ameuhitaji. Kuwa na uhakika na Mungu, na kisha ushikilie, timiza masharti Yake. Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo ambayo ni sahihi, anajua jinsi ya kuyafanya kwa njia sahihi.

62 Sasa, ni jambo la kushangaza sana kwamba Mungu angemtuma nabii wake kwenye nyumba ya mwanamke mjane. Ni mahali pa jinsi gani! Lakini hapana shaka alikuwa ni mwanamke mwema kweli, la sivyo Yeye asingemtuma nabii Wake hapo. Loo, ikiwa mtu anastahili, inabidi awe ni mtu anayestahili kumkaribisha mtu kama Eliya.

63 Unakumbuka, ilikuwa Zekaria, nyumbani kwake, ambaye alikuwa mwaminifu na wa kweli, akingojea Mungu awape mtoto, na Malaika, Gabrieli, alikuja nyumbani. Ilikuwa ni bikira Mariamu ambaye alikuwa ameishi maisha safi na yasiyo na doa, na akingojea ahadi ya Mungu, ambaye Yeye alimtumia Malaika.

64 Unaongea juu ya kuzunguka na ulimwengu na kubembana na ulimwengu, na kisha unatarajia kuona malaika na kufanyiwa miujiza, yako nje ya mpango wa Mungu. Lazima uishi sawa. Safisha nyumba, safisha tabia zako, safisha mambo ya ulimwengu, ondoa karata zako na ushirika wako wa kidunia, jiandae, na ndipo Malaika wa Mungu anaweza kuzungumza na kusema, “Usiogope, ni Mimi.” Kisha mambo yanafanyika. Lakini yeye . . .

65 Maskini yule mwanamke alikuwa akiomba, bila kujua kwamba akitembea chini ya mlima alikuja nabii. Alikuwa ameona ono, pa kwenda. Mungu hawaongozi watu wake kiupofu, anawaambia wanakoenda. Alikuwa akiangalia mjini. Loo, ilikuwa mbaya. Watu walikuwa wanakufa kwa njaa, na

wakililia maji, na watu wenye njaa. Ni dhihirisho la ukosefu wa maadili. Ni dhihirisho la dhambi.

66 Na taifa hili litajuta. Huwezi . . . Mizani, hata kanuni ya maumbile haingeruhusu iwe hivyo, wakati tuna—wakati tunapopoteza pesa kwa maisha ya fujo, na nusu ya ulimwengu inakufa kwa njaa (wote ni wanadamu ambao Kristo alikufa kwa ajili yao).

67 Hiyo ndiyo sababu uwanja wa misheni uko moyoni mwangu. Mna wahudumu wazuri hapa Phoenix, na kote Marekani na sehemu zingine, makanisa kwenye kila kona, watu mashuhuri wa Mungu, ibada za uponyaji, watu mashuhuri kama Oral Roberts na watu wengine mashuhuri, wakihubiri. Na kuna watu kule, wanaokufa kwa maelfu kila siku, ambao hawajasikia kamwe Jina la Yesu. Maskini wanegro wadogo, wachafu, wenye njaa, huko chini huko Afrika na kule India, jamaa wadogo wamelala barabarani, wakifa, hata hawajui "Mungu" maana yake nini. Na kisha tunabishana juu ya tofauti zetu kidogo za imani ya kidini. Loo, sio sawa kabisa (sidhani, marafiki), ikiwa moyoni mwako kuona hiyo.

68 Sasa, angalia maskini mwanamke huyu mdogo, baada ya kuchungulia dirishani na kuona kwamba ilikuwa karibu kupambazuka, hakujua ni nini kilikuwa kinamsubiri. Alikuwa anafikiria ilikuwa ni kifo kwake na kwa mvulana wake mdogo. Kwa hivyo mimi . . . Wakati amelala, wacha tu tumtazame kwa dakika chache. Yeye anaenda, akiisha kuomba, na yeye anapiga maskini nywele zake kutoka kwa macho yake, na kusema, "Mpenzi mwanangu, unaonekana sana kama baba yako wa thamani, mtakatifu. Jinsi alivyomtumaini Mungu! Jinsi alivyojitoa maisha yake kwa sababu ya Israeli, nje kwenye uwanja wa vita! Na wewe unafanana sana naye. Na, Mpendwa, sijui ni kwa nini wasio na hatia wanateseka na wenye hatia, lakini wanateseka."

69 Taifa hili, Wakristo, watateseka kwa sababu ya ukosefu wa haki katika siasa, utafanya taifa lote kuteseka.

70 Sasa ninaweza kumwona akiingia na kusema, "Nitatengeneza keki kidogo sasa. Nina ya kutosha tu kwa keki moja ndogo ya—ya mkate uliobaki, na tukishaila, ndipo tutakufa." Kwa hivyo anaingia chumbani, na kuchukua unga kutoka kwenye pipa la unga. Ninaweza kumuona akilifuta tu kutoa vumbi kwa mkono huo mdogo, wenye mifupa, huku akipiga kipipa ambacho kilikuwa ndani yake; akikipiga, kila vumbi, na mwishowe akapata ya kutosha tu kwa ajili ya keki moja; anaenda huko kwenye chupa ndogo na kuiinua juu na kutoa kila mafuta kidogo ndani yake, yapata kijiko kimoja kilichojaa.

71 Sasa, unga, vitu hivyo vyote vina maana. Unga ulimwakilisha "Kristo." Kristo alikuwa ndiye sadaka ya unga.

Waliposaga unga kwa ajili ya sadaka ya kutikiswa, kwa ajili ya Kristo, ambaye alikuwa Kristo katika sadaka ya kutikiswa, katika Agano la Kale, waliisaga na aina fulani ya kinoo, ambapo kila kipande kidogo cha unga lazima kikatwe sawa, kwa sababu Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

72 Unakumbuka wakati baadhi ya shule huko juu hazikujua tofauti kati ya matango na njegere, na kutupa baadhi ya matango mwitu ndani ya supu ya njegere, kupika, wakalia, "Kuna kifo kwenye chungu."

73 Eliya akatwaa konzi ya unga, akatupa ndani ya chungu, akasema, "Kuleni!" Unga huo ulifanya nini? Unga, kwenye chungu, uliyabadilisha kutoka mauti yakawa uzima; kutoka kwa rasilimali inayoleta kifo hadi rasilimali inayoleta uhai.

74 Hivyo ndivyo ilivyo usiku wa leo, wakati kuna kifo kwenye chombo chako. Kristo, akitupwa ndani ya chombo chako, hukutoa kutoka mautini hadi Uzimani. Kristo huleta tofauti. Akija ndani ya moyo wa mwanadamu, loo, Yeye hutoa amani ipitayo ufahamu. Na pia hutoa Uzima wa Milele, "Yeye amwaminiye Mwana yuna Uzima wa Milele, naye hataangamia kamwe."

75 Sasa, alichukua unga, ambao ulimwakilisha Kristo. Naye Kristo ndiye Neno. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu." Kristo, sadaka ya Unga! Kisha akaenda na kuchukua mafuta. Na *mafuta* yanawakilisha "Roho." Kwa hivyo aliweka Neno na Roho pamoja, na kuanza kuvichanganya.

76 Loo, jambo fulani halina budi kutokea wakati hilo linapofanyika! Acha iwe usiku wa leo ambapo Neno ambalo ninahubiri litaangukia moyoni mwako. Basi acha Roho Mtakatifu aingie hapo na aanze kuchanganya Hilo. Angalia kile kinachofanyika unapoweka Neno na Roho pamoja! Yesu alimwambia yule mwanamke kisimani, "Mwanamke, ninakwambia, wakati unakuja, na sasa upo, ambapo Mungu anahitaji kuabudiwa kwa Roho na Kweli." Na Yeye ndiye Kweli.

77 Unga, angalia kile alichofanya, alichanganya Neno na Roho pamoja. Watu wengi wana Roho bila Neno, wengine wana Neno bila Roho. Lakini wewe chukua, weka Zote mbili kwa usahihi mahali pao, kuna keki njiani! Kuna kitu kinakuja.

78 Maskini mjane huyo mdogo hakujua alichokuwa akifanya, lakini Mungu alimwambia Eliya, "Nimemwamuru."

79 Naye Eliya yuko njiani juu ya mawe, akija chini kuona ono lake likitimizwa mahali pengine. Na hapa mwanamke huyo amesimama pale, anafuta machozi kwa maskini mkono wa vazi lake uliochakaa, na kusema, "Ee Yehova Mungu, imani yangu haijawahi kushindwa kamwe, wala haitashindwa. Kwa namna fulani au nyingine, sijui jinsi hii yote ilivyo, lakini

tunafundishwa kuwa vitu vyote hufanya kazi pamoja kwa wema." Alikuwa akichanganya unga huu kidogo, aliiandaa keki hiyo ndogo kabisa na kuiweka tayari. Alisema, "Sasa ni wakati wangu kwenda nje na kutafuta kuni." Anarudi na kufungua mlango, akasema, "Ee Bwana, maskini tumbo lile lenye njaa limelala hapo, na sijala kwa wiki mbili au tatu. Nimempa kipande changu cha keki."

80 Huyo ni mama, upendo wa mama kwa mtoto wake. Hakuna kitu kama huo, ila tu upendo wa Mungu. "Mama anaweza kumsahau mtoto wake anayenyonya, bali mimi siwezi kuwasahau kamwe. Majina yenu yamechorwa kwenye vitanga vya mikono Yangu." Anawezaje kukusahau? "Sitakuacha kamwe, au kamwe kukuacha. Nitakuwa pamoja nawe daima, hata kufikia mwisho wa ulimwengu."

81 Huko anamtazama mtoto wake mchanga, labda alirudi nyuma na kubusu maskini paji la uso wake. Kama huenda alizimia na kufa nje huko. Anatoka nje. Imeanza tu kidogo kama vile . . . jua linaanza kuchomoza juu ya milima ya Uyahudi. Naye anaangalia jua likianza kutokeza. Chini huko barabarani anasikia kulaani na kuendelea. Basi anaenda huko uani na, angalia, alichukua vijiti viwili (sio vilivyojaa mkono), vijiti *viwili*. Ni nini hiyo? "Msalaba."

82 Sasa, mtu yeyote anajua, yeyote wa rafiki zangu wa Kihindi hapa anajua, au mwindaji yeyote, njia sahihi ya kufanya moto kudumu, ni, kukingama vijiti viwili, magogo mawili, uwashe moja kwa moja katikati, na uendelee tu kusukuma miisho yake iingie. Utadumu usiku kucha. Mara nyingi nimelala nyikani, na vijiti viwili si vikubwa kuliko *hicho,* na kudumisha joto usiku wote. Wa kutosha tu kudumisha joto, kuufanya uendelee moja kwa moja katikati yake.

83 Sasa atafanya nini? Kuwasha vijiti hivi viwili. Na Neno na Roho wameleta dhabihu ya kujitolea msalabani, tayari kwa jukumu, tayari kwa maisha. Kuweka Neno na Roho, hiyo ni imani yake katika Neno la Mungu kwa Roho Mtakatifu, akijiongoza mwenyewe kutoa dhabihu kitu chochote kingine Msalabani. Na wakati alipochukua kijiti chini ya mkono wake, viwili, na kuanza kurudi, alianza kurudi, na kulikuwa na sauti iliyosikika kutoka langoni, "Mama."

84 Kabla tu ya hapo, mzee, labda mwenye upara, na mvi zikining'inia juu ya masharafa yake, na nywele zake zikining'inia chini, fimbo ndogo mkononi mwake, maskini ngozi ya kondoo au kitu fulani alichojifunika, akitembea barabarani, akisema, "Bwana, ni uzio mdogo mweupe. Kutakuwa na mwanamke mdogo anayeonekana wa kupendeza" (lazima alikuwa mchanga, mvulana huyo alikuwa mchanga) "nje uani. Uliniambia huyo ndiye mjane ambaye alikuwa anilishe. Sasa, yuko wapi? Nitaendelea kutembea." Roho anamwongoza njia

*hii*, kisha humgeuza. Loo, ni ajabu sana kwani wana wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu. Haijalishi inasikika ya kijinga jinsi gani, wanaongozwa! Yeye anaenda. . . Anashuka barabara moja na kwenda nyingine, chini ya barabara moja na kupanda nyingine.

Baada ya muda, Roho akasema, "Angalia upande wako wa kulia."

85 Naye anaiangalia kote namna *hiyo,* kama vile tu Yeye hufanya hapa jukwaani, usiku baada ya usiku. Loo, Mungu angali ni yule yule! "Angalia upande wako wa kulia, upande wako wa kushoto, kuna mtu anayeomba anayeuhitaji."

86 Na akatazama upande wake wa kulia. "Aise, huo hapo uzio mdogo mweupe. Hiyo ni sawa tu. Sitatoka hapa, kwa sababu kuna mti wa zamani umesimama pale. Na hapo kila kitu kipo jinsi tu nilivyoona katika ono." Mlango unafunguka na maskini mwanamke mwembamba anatoka nje.

87 Sasa, kumbukeni, atachukua vijiti viwili tu. Hangeweza kuchukua vitatu, anachukua viwili kutengeneza Msalaba. Aliokota vijiti viwili na kuvitia mkononi mwake na akaanza kurudi, akiwazia, "Nitaoka keki kidogo wakati mwanangu atakapoamka. Na kisha nitamlisha hiyo, mimi sitakula yoyote. Nami nitamweka maskini mvulana wangu mikononi mwangu, na hapo tutaketi na kufa." Akaanza kuingia ndani ya nyumba.

88 Alisikia sauti ya ajabu kupitia langoni, ikasema, "Mwanamke, unaweza kuniletea maji kidogo kwenye chombo?"

89 Akageuka, akawazia, "Yule pale mzee mwema amesimama langoni." Alimtazama kwa karibu sana, na labda akafuta machozi kutoka kwa macho yake, ilikuwa mapema sana bado. Unajua, Mungu hufanya mambo kiajabu sana. Alikuwa tayari kujitolea. Maji yalikuwa kitu adimu, mvua haikuwa imenyesha kwa miaka mitatu na miezi sita.

90 "Naomba uniletee mimi. . ." Labda Mungu alimwambia aseme hivyo, aone kile mwanamke huyo atakachofanya, kujaribu majibu yake. "Je, unaweza kuniletea maji kidogo ya kunywa kwenye chombo?"

91 Naye akamwangalia. "Anasikika tofauti. Kuna kitu kuhusu mzee huyo ambacho kinanitia huruma."

92 Mwaminio yeyote katika Mungu atamgawia mwingine hadi cha mwisho. Naam. Hilo ni jambo moja kuhusu watu wa Pentekoste, watatoa shati mgongoni mwao na kumpa mtu, kwa ajili ya Huduma. Hiyo ni kweli. Ni ukweli. Hilo ni jambo kuu, moja ya mambo makuu waliyo nayo. Wao ndio watoaji wakuu zaidi ulimwenguni, maana wanajua kwamba mali hii ya dunia si kitu. Wanaweka hazina zao Mbinguni, maana wanaenda huko baadhi ya siku hizi.

93 Na kwa hivyo mwanamke huyu, alisema, "Nitayashiriki tu maji yangu na mwingine. Tutakufa, kwa hivyo nitajinyima maji yangu ya kunywa, na kumpa yule mzee mwenye fadhili aliyesimama pale, kwa sababu anaonekana mwenye kiu na mchovu." Akasema, "Nitayaleta." Ndipo akaanza kutembea.

94 Tena akasikia sauti, ikisema, "Na kwa mkono wako mwingine, waweza kuniletea mkate kidogo?" Loo, jamani! Sasa, sasa kitu gani?

95 Tumaini lake la mwisho la maisha ya mtoto wake. Tumaini la mwisho walilokuwa nalo, na mkate ungemalizika, mafuta yangeisha, kila kitu kingekwisha sasa. Lakini aliangalia nyuma, na akashangaa. Akasema, "Nina unga kidogo tu kwenye pipa. Nina mafuta ya kutosha tu ambayo nimeyapunguza, na tayari nimeyatayarisha, au, nimechanganya. (Nina Neno na Roho vimechanganyika pamoja huko ndani. Nina Msalaba hapa kuiwekelea, kuifanya keki ili kuleta Uzima.)" Na hapo ndipo wakati Roho na Neno wanapokutana, pale Msalabani, hufanya mkate wa Uzima kwako. Hiyo ni kweli. "Nami nimeiunganisha, na ninaingia sasa kuioka, na kumpa mvulana wangu mdogo anayekufa mle ndani, ambaye amelia usiku kucha kupata kitu cha kula, si—sina budi kumpa. Nitajinyima yangu na ni—nitampa yeye. Na kisha nitamchukua mikononi mwangu, na sote wawili tutasubiri kifo."

96 Akasema, "Lakini, wewe niokee moja ndogo, kwanza." Hiyo si ni ajabu kwamba mwanamume angemwomba mjane, anayekufa, ampe chakula cha mwisho alichokuwa nacho nyumbani, huku ana mtoto anayekufa? Mungu hufanya mambo kiajabu sana! Kasema, "Niokee moja ndogo, kwanza!"

97 Alisoma, "Unajua, Biblia inasema kwamba tumekaribisha wageni. Tumewakaribisha wageni, walikuwa malaika, bila kujua tulichokuwa tunafanya." "Vema," akasema, "Nitafanya hivyo."

98 Na alipogeuka, akasema, "Kwa maana . . ." Loo, jamani. Hiyo hapo, faraja kubwa zaidi ambayo mwaminio yeyote aliwahi kusikiliza, "Kwa maana, BWANA ASEMA HIVI!" Hilo ndilo Neno ambalo alikuwa akingojea. "BWANA ASEMA HIVI, 'Pipa halitapungua, wala chupa haitaisha, hata siku ile Mungu atakapoleta mvua juu ya nchi.'"

99 Tunapata nini hapo? Tafuteni kwanza Ufalme wa Mungu, na haki Yake, vitu vingine vyote vitaongezwa. "Ninajuaje, Ndugu Branham? Ninajuaje?" Kitu pekee ninachojua, mtangulize Mungu na usonge mbele. Kujitoa! Changanya mafuta, changanya Ne—Neno na Roho pamoja, jiweke Msalabani, na useme, "Mimi hapa, Bwana." Mtangulize Mungu katika kila jambo!

100 "Kwa kuwa, BWANA ASEMA HIVI, 'Chupa haitaisha, na pipa halitapunguka, mpaka siku ile Bwana Mungu atakapoleta

mvua juu ya nchi.'" Alijua, basi, huyo alikuwa ni nabii wa Mungu akizungumza naye. Loo, jinsi moyo wake hapana shaka uliruka! Aliingia mbio na kutengeneza keki hiyo ndogo na kumletea, na maji, mikono inayotetemeka juu ya maskini mashavu hayo yaliyobonyea, alijua kwamba Mungu alikuwa amekuja kuwaokoa, kwa kipande kidogo cha mkate.

101 Loo, wewe chukua tu hiyo ahadi moja ndogo ya Mungu, na uweke kila kitu sawa, na ukiondoe njiani, uone kinachofanyika! Ondoa moyo huo. . .kutokuamini mbali nao. Chukua tu imani hiyo ndogo uliyo nayo, na uiweke juu ya Msalaba, na useme, "Hii ndiyo yote niliyo nayo, Bwana. Ichukue"; angalia badiliko, "BWANA ASEMA HIVI." Loo, Yeye ni yule yule leo kama alivyokuwa daima. Hilo ndilo alilokuwa akingojea.

102 Labda kunaonekana giza sana sasa, lakini, unajua, wakati mwingine tunafundishwa (na nilihubiri juu yake hivi majuzi usiku) kwa kawaida huwa giza kabisa kabla ya mapambazuko. Ni katika saa yenye giza kuliko zote ya usiku ndipo nyota ya asubuhi huangaza, inaakisi kuja kwa jua.

103 Huko Ujerumani wanayo picha, wanaiita picha ya "Wingu". Ni—ni ushindani dhidi ya picha hii nzuri ya kusulubiwa huko kwenye. . .kwenye Forest Lawn huko Los Angeles (picha hiyo mashuhuri ni pana kama jengo hili kutoka upande mmoja hadi mwingine, iliwabidi kujenga jengo kuizunguka hiyo picha; wengi wenu mmeiona). Lakini hii huko Ujerumani inaitwa, "malaika. . . " au, "Siku ya Wingu," ninaamini ndivyo inavyoitwa. Na unapoachana na kijipande kutoka kwake na kukiangalia, loo, kinaonekana cha kutisha, inaonekana kama mawingu yenye hasira yakichanganyana, namna hiyo, wakati nuru zinapoiangazia. Na inaonekana kana kwamba mawingu yanasonga, kwa vile picha imetengenezwa kuakisi nuru, kuifanya ionekane kama wingu, dhoruba yenye hasira inayokuja kubomoa kila kitu. Na kisha unaambiwa na kiongozi, "Sogea karibu, na uendelee tu kuitazama." Na unapofika karibu sana nayo, si mawingu, ni mabawa ya malaika yanayopiga pamoja, wakifurahi. Ni baraka iliyojificha.

104 Labda ugonjwa wako usiku wa leo, labda kujitolea kwako kuja hapa, kulikuwa baraka tu kwa njia iliyofichika. Malaika wa Mungu wapo hapa, wapo, kuunganisha mabawa yao pamoja na kufurahi, kwa sababu imeandikwa katika Maandiko, kwamba, "Malaika wa Mbinguni hufurahi wakati mwenye dhambi mmoja anapotubu." Fikirieni juu ya hilo. Kwa maana, BWANA ASEMA HIVI, Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Neema yake haiwezi kumalizika. Na Yeye yuko tayari kuwapa chochote ambacho mioyo yenu inataka.

105 Sasa hebu tuombe kwa muda, wakati tunapoinamisha vichwa vyetu kwa maombi. Na ninatumaini kuwa mtakaa katika hali ya kuomba. Je, kuna mtu hapa sasa (huku macho

yenu yamefumbwa na vichwa vyenu kuinamishwa kuelekea kwenye vumbi ambapo mlichukuliwa kutoka; na, Yesu akikawia, mnarudi mavumbini) nawe hujaokoka, je, waweza kuinua mkono wako kiasi *hicho*, na kusema, "Ndugu Branham, maisha yangu yamekuwa taabu, pia, na sijaokoka. Unikumbuke katika maombi yako usiku wa leo, Ndugu, nitainua mkono wangu"? Je, mtu huyo yupo hapa ndani, mvulana, msichana, mwanamume au mwanamke, ambaye hajaokoka? Sitakuuliza zaidi, kuinua tu mkono wako sasa ili niweze kukuombea.

106 Mkono wangu wa kulia, Mungu akubariki, Mungu akubariki, Mungu akubariki, na wewe, na wewe. Mahali pengine, nyuma kabisa upande wa nyuma, mahali fulani hapa kwenye marefu ya katikati, inua tu mkono wako. Hakuna anayeangalia, acha tu mimi na Roho Mtakatifu tuangalie. Sasa, Mungu akubariki, Mungu akubariki. Hiyo ni nzuri.

107 Mtu mwingine katikati ya marefu, inua mkono wako, useme, "Ndugu Branham, mimi si Mkristo. Ni—nimemchosha Roho Mtakatifu mbali sana na mimi mpaka Yeye hata hanisumbui tena. Lakini, kwa kweli, najua kuwa nimekosea. Najua sijawahi kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu. Najua kwamba mimi—mimi sifai. Sina ninii yoyote. . .Sijaungama mambo yangu yote. Sijatimiza masharti yote ya Mungu."

108 Labda wewe ni mgonjwa. Haitasaidia chochote mpaka utimize masharti ya Mungu. "Ndugu Branham, nimekiri Ukristo muda mrefu, lakini kwa kweli daima nimetilia shaka uponyaji wa Kiungu. Kwa namna fulani ni—nimejiuliza tu kama huyu Roho Mtakatifu alikuwa sahihi." Loo, dada mpendwa, au, ndugu mpendwa, huwezi kupata chochote kutoka kwa Mungu kwa njia hiyo. Hapana. Lazima utimize kila sharti, na kisha uwe na hakika kuwa uko sawa na Mungu. Kisha uchukue ahadi Yake na uishikilie.

109 Mkono wangu wa kushoto, kunaweza kukawa na wengine huko ndani? Baadhi yenu vijana huko nyuma, kadri ilivyo, ikiwa wewe si Mkristo, inua mkono wako na useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham." Mungu akubariki, naona mikono yenu, nyuma kabisa ndani, nyuma kabisa upande wa nyuma, nakuona, mama; nyuma hapa, ndiyo. Huku, mbali hapa, ndio, msichana huyo mdogo. Naam, naam Bwana akubariki kila wakati huko. Hiyo ni nzuri.

110 Sasa, niliwaahidi huku nje hayo ndiyo tu ningewauliza, kuinua tu mikono yenu. Sasa tunaenda kuomba. Na kabla ya kufanya hivi sasa (baada ya kuwafanya wenye dhambi kuinua mikono yao, watu ishirini au thelathini), ni wangapi wagonjwa, ungeinua mkono wako na kusema, "Nikumbuke, Ndugu Branham, katika maombi yako, kwamba Mungu atanirehemu na kuniponya"? Nadhani kuna mia mbili, au zaidi, wa hao. Sawa.

Na tuombe.

111 Baba yetu wa Mbinguni, ni neema sana kuja Kwako na haja hizi. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] "...na Kwangu, mimi ni Muumba wako." Nao wakainua mikono yao, basi hiyo inaonyesha kwamba Roho ni mkuu kuliko sayansi. Baba, Wewe ulisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, isipokuwa Baba Yangu amvute kwanza. Na wote wanaokuja Kwangu, nitawapa Uzima usio na mwisho." Sasa hao ni Wako, Bwana. Wape Uzima, sasa hivi, mahali wanapoketi kwenye viti vyao. Wajalie kuwa na Uzima wa Milele. Naomba uwainue siku ya mwisho, uwawasilishe kwa Baba Mungu wa Mbinguni kama vito katika taji ya Kanisa. Ijalie, Baba.

112 Ninawaombea hawa ambao ni wagonjwa na wanaoteseka. Mikono yao mingi iliinuliwa usiku wa leo, kwa sababu waliona kwamba mwanamke aliyehitaji Mungu sana; aliona saa hizo muhimu zikija. Hapana shaka kuna wengi wameketi hapa kwa njia iyo hiyo, ambao hawana budi kufa, lakini tayari Mungu amewaamuru manabii Wake, na kila kitu ni sawa. Kitafanya kazi vizuri tu. Ikiwa wana hakika kuwa kila kitu ni sawa, basi wana uhakika na Mungu. Wana hakika kwamba Yeye hutimiza ahadi Yake. Halafu, Baba, tunaomba kwamba utashughulika nao usiku wa leo, kama watoto wako wapendwa, wagonjwa; na utayaponya mateso yao, na kuwapa nguvu na neema na imani. Fanya hivyo, Baba.

113 Wabariki wahudumu wote walio hapa usiku wa leo, manabii wako wa thamani. Tunaomba kwamba utawatia mafuta, Bwana, na wawe wao ndio watakaobariki nyumba za watu hawa, kwamba kutakuwa na Mkate wa Uzima katika nyumba zao maadamu wanaishi. Chupa yao na isiishe, wala mapipa kupungua. Jalia kuwe na mkate wa kiroho katika kila kanisa kote katika nchi hii, Bwana, ambao utawalisha wenye njaa ambao ni wahitaji. Lijalie, Bwana.

114 Tunakupenda. Nasi twajua ya kuwa Wewe ulitupenda kwanza, kwa maana wakati tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu, Asiye na hatia kwa ajili ya wenye hatia, kuwa upatanisho wa dhambi zetu, kutupatanisha tena na Mungu; wakati tulipokuwa tumepotea na katika shida, bila Mungu wala Mwanawe, kutoka bustani ya Edeni, kutokana na makosa ya baba zetu yaliyotuleta katika machafuko ya dhambi. Na Yesu alitupenda sana hivi kwamba alikuja kwa mapenzi ya Mungu na kutukomboa aturudishe kwa Mungu, kupitia sadaka ya maisha Yake mwenyewe pale Kalvari. Asante, Baba, kwa wema Wako wote.

115 Tunaishi katika vivuli vya wakati wa mwisho. Huenda kusiwe na kesho usiku. Sijui, Bwana, hiyo ni Kwako. Lakini wakati bado inawezekana kwamba wengine wanaweza kuingia usiku wa leo, Baba, naomba kwamba Wewe utamtuma Roho Mtakatifu.

116 Ulisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu." Katika siku za Sodoma, walikuwa na matabaka matatu ya watu: mwenye dhambi, mshiriki wa kanisa mwenye uvuguvugu, na Wateule (walioitwa watoke); Wasodoma, na wa Lutu, na wa Ibrahimu (walioitwa kutoka ulimwenguni). Wasodoma walipokea wahudumu wawili na ujumbe mashuhuri. Na kikundi cha Ibrahimu kilipokea ishara, na ishara ilikuwa Mtu mwenye vumbi kwenye nguo Zake, ambaye alimjua Ibrahimu, huku ni mgeni; alijua mkewe, Sara, jina lake ni nani; na, akamwambia Ibrahimu, huku amegeuza mgongo Wake kwenye hema alipokuwapo Sara, "Kwa nini alicheka?" Ee Mungu, kanisa na liamke na kuona! Kama Yesu alivyosema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa wakati wa kuja kwake Mwana wa Adamu." Mungu yuyo huyo angeonekana katika mwili wa Kanisa Lake, na angeonyesha ishara hiyo hiyo. Ijalie, Bwana, tena usiku wa leo. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, nampenda

Sasa mwabudu Yeye tu kwa utamu katika Roho.

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

117 Loo, baada ya ujumbe, hivi hamjihisi tu kusuguliwa kabisa? Ni Roho Mtakatifu tu anayesafisha moyo wako kutokana na kutokuamini kwote, akurudishe tena katika njia pamoja na Mungu. Loo, sasa ni wakati wa kumwabudu Yeye. Ujumbe umeisha, kwa hivyo hebu tumwabudu tu Yeye mara nyingine tena katika wimbo huu, tunapoimba *Nampenda*. Kila mtu, kwa utulivu tu na kwa utamu sasa. Funga macho yako na uangalie tu kwa macho yako ya kiroho kuelekea Kwake, angalia kile Yeye alichomfanyia mjane huyo. Wewe ni mpendwa Kwake kama yule mjane, amehifadhi maisha yako, pia. Hivi humpendi?

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Tabibu mkuu yu karibu sasa,
Yesu mwenye huruma,
Ananena ili kuchangamsha moyo wenye huzuni,
Hakuna jina jingine ila Yesu.

Sauti nzuri sana katika wimbo wa kimalaika,
Jina tamu zaidi kwenye ulimi wa mwanadamu,
Wimbo mtamu sana wa furaha uliowahi kuimbwa,
Loo, Yesu, Yesu wa thamani.

118 Wakati anaupiga kwenye kinanda, polepole. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Tabibu Mkuu*—Mh.] Ninaposikia wimbo huo, unaleta jambo moja kwangu. Wakati fulani uliopita huko Ft. Wayne, Indiana, kulikuwa na msichana mdogo wa Dunkard ameketi, akipiga piano. Yeye hakuwa Mpentekoste, lakini alikuwa na nywele ndefu nzuri zilizofungwa nyuma. Nami nilikuwa ninaenda kuwaombea wagonjwa, na wa kwanza kwenye foleni alikuwa mvulana mdogo, alikuwa mlemavu, kisa cha polio. Ndipo nikamchukua mvulana huyo mdogo kutoka mikononi mwa dada huyo, na kumshika maskini mvulana huyo, nikasema, "Kweli, Tabibu mkuu yupo hapa, anajua siri za mioyo yote."

Nikasema, "Mnaamini hilo?" kwa kusanyiko la watu elfu kadhaa.

119 "Naam," wote waliliamini. Lakini kidogo walikuwa wakizuia, ulikuwa usiku wa kwanza wa mkutano, nao walikuwa . . . Ujumbe ulikuwa mgumu kwao kuelewa.

120 Ndipo nikasema, "Je, mnaamini kwamba Bwana Yesu anaweza kuniambia huyu mvulana mdogo ni nani, na jina lake ni nani? Je, mtaamini? Je, huyo angekuwa ni Malaika yule yule aliyekutana na Ibrahimu, aliyejua kile Sara . . . Je, ingekuwa ni Yesu yule yule aliyemjua Nathanaeli alipokuja, aliyemjua Petro na kumwita kwa jina, aliyemwambia yule mwanamke kisimani, na mambo haya yote? Je, huyo angekuwa Yesu yule yule?" Wote waliinua mikono yao, walidhani itakuwa hivyo.

121 Ndipo Roho Mtakatifu akaanza kufunua hili. Na, alipofanya hivyo, yule mvulana mdogo aliruka kutoka mikononi mwangu, akakimbilia chini na akaruka kutoka jukwaani. Mama yake alizimia kwenye kiti ameketi moja kwa moja mbele ya yule mvulana mdogo. Na yule mvulana mdogo akikimbia huku na huko. Msichana wa Amishi, au Dunkard alikuwa, akipiga piano, aligeuka mweupe kabisa, akaruka juu katika—katikati ya mkutano, na nywele zake zikaanguka mgongoni mwake. Alikuwa amevaa nguo nyeupe. Alionekana kama malaika. Naye akaanza kuimba huo katika lugha zisizojulikana. Na, alipofanya hivyo, piano haikukosa sauti yoyote, ikipiga:

> Tabibu mkuu yu karibu sasa,
> Yesu mwenye huruma,
> Ananena ili kuchangamsha mioyo yenye huzuni,
> Hakuna jina jingine ila Yesu.

122 Watu walimiminika chini kuzunguka madhabahu, na kulia na kuanguka kwenye marefu, na kupiga mayowe "Mungu nirehemu!" Loo, kulikuwa na mkutano wa jinsi gani!

123 Tabibu huyo mkuu bado yuko hapa. Hajashindwa. Hawezi kamwe kushindwa. Sasa, ni wangapi hapa wanaoamini jambo

hilo, kwa dhati, kwa moyo wako wote, nawe uko hapa usiku wa leo na matarajio ya kuponywa kwa nguvu za Mungu?

124 Ikiwa kuna mtu yeyote ndani ya jengo ninayemjua, nje ya hawa papa hapa, wavulana hawa walioketi hapa, watatu kati yao ambao niliongea nao hivi majuzi kwenye mahojiano, kutoka Arkansas; Ndugu Pat Tyler, ambaye ni jambazi aliyeongoka; Ndugu Williams anayeketi pale pale; na kadiri niwezavyo . . . na Ndugu Gene Goad, sahibu wangu, aliyeketi papa hapa. Na ninadhani hao ndio tu ninaowaona katika jengo ambao ninawajua kwa wakati huu, lakini huku ninawajua watu hawa wanaoketi hapa.

125 Sasa, nimesimama na Korani kwa mkono mmoja, na Biblia kwa huo mwingine, mbele ya watu laki moja, na kusema "moja haina budi kuwa sahihi, na hiyo nyingine uongo." Na dini ya Kikristo ndiyo pekee kati ya dini zote; na Full Gospel ndilo kundi pekee kati yao linaloweza kuthibitisha kwamba Yesu Kristo bado anaishi. Wengine wote wana theolojia, na watakuambia juu yake, "Tuna saikolojia nyingi tu hivyo." Waislamu wanasema, "Tuna saikolojia nyingi. Tunaweza kupaza sauti kwa sauti kubwa juu ya nabii wetu kama vile mnavyoweza juu ya Yesu wenu. Lakini nabii wetu hakuwahi kutuahidi chochote. Yesu wenu aliwaahidi kwamba atafufuka kutoka kwa wafu, na mambo ambayo Yeye alifanya mngeyafanya pia kwa sababu Yeye angeishi ndani yenu. Sasa mnasema nabii wetu amekufa, huko nje kaburini, nanyi mnaye Yesu aliyefufuka. Hebu tumwone akitenda." Wataweka . . . usininii . . .

126 Unaweza kucheza hapa na baadhi ya wanatheolojia hawa, juu ya maneno kadhaa ya Kiyunani au kitu ambacho wewe mwenyewe umechanganyikiwa kabisa juu yake, lakini usijaribu kamwe kuleta shindano na baadhi ya watu hao. Afadhali uwe na kile unachozungumzia. Na heri ujue. Ndiyo sababu ni vigumu kupata wamishenari huko. Wanajua wanachokizungumzia. Na ni heri ujue, kwa sababu watakupa changamoto juu yake.

127 Lakini nashukuru sana usiku wa leo, kujua, marafiki, kwamba Yesu wetu (na kila ahadi aliyotoa) ni Kweli. Ikiwa ningeweza kumponya mtu yeyote hapa, ningefanya hivyo; kama nisingefanya hivyo, ningekuwa mnafiki. Lakini siwezi. Lakini Mungu amelipa kanisa karama, ambayo aliahidi.

128 Kwamba katika siku za Luther, tuliishi kwa kuhesabiwa haki. Katika siku za Wesley, tuliishi kwa utakaso, kanisa likawa katika uchache. Katika siku za Pentekoste, tumeishi kupitia Ubatizo wa Roho Mtakatifu na kurejeshwa kwa vipawa. Sasa tuko katika uchache kabisa, kuja kwa Mwana wa Mungu. *Hapa* waliamini kwa imani; *hapa* walipiga kelele chini ya utakaso; *hapa* walinena kwa lugha kama karama; lakini *sasa* kivuli na cha halisi, na ki—kifuniko kinakuja juu ya piramidi, na ni wakati wa mwisho, wakati Kristo na kanisa Lake wanafanana sana

hata itaita wafu kutoka kwa Wamethodisti, Walutheri, na wale wote huko nyuma, na kutakuwa na ufufuo. Wale waliolala katika zamu ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita, na ya saba, watafufuka moja ya siku hizi, kukutana na Yesu angani. Saa imewadia, marafiki, Kuja kwa Bwana kumekaribia.

129 Tunatazama Yerusalemu na kuona kwamba Wayahudi walipofushwa kwa ajili yetu. Mtini unachipusha matawi yake. Alisema, "Na miti mingine." Billy Graham amesababisha u—uamsho kati ya watu baridi. Oral Roberts amesababisha uamsho kati ya Wapentekoste. Na sasa Yesu, Mwana wa Mungu, amekuja kwa mabaki haya, kuwavuta watu kwa ajili ya Jiwe la kifuniko, kumrudisha Mwana wa Mungu, kukamilisha jambo hilo kwa ajili ya Kuja kwa Bwana Yesu. Alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwa Mwana wa Adamu."

130 Nitawageuzia mgongo wangu, sio tu ili mwone. Sasa, kumbuka, hakuwa yule mtu. Mtu aliyekuwa ameketi pale alikuwa tu ni kalisi, potashi, na petroli, elementi kumi na sita za ulimwengu ambazo Mungu alifanya, "Phew!" zikapulizwa pamoja na akaingia ndani yake na akaishi.

131 Yesu Kristo alikuwa ni kitu kile kile. Alikuwa Mwana wa Mungu. Alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, lakini mwili wake ulikuwa mwanadamu, Roho Wake alikuwa Mungu. Ndipo akaahidi katika siku za mwisho kwamba atakuja katika Kanisa Lake. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena; bali nyinyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Kazi nizifanyazo Mimi nanyi mtazifanya pia." Unaona? Sasa huyo Tabibu mkuu yupo hapa.

132 Akasema, sasa, "Ishara ya Sodoma na Gomora." Sasa, ni nini? Angalia magazeti yetu, "Mashoga, upotovu, unaongezeka kwa asilimia arobaini zaidi ya miaka kumi iliyopita." Matetemeko ya ardhi mahali mahali, aina zote za ishara za Kuja. Kanisa linaanguka, wakati wa mwisho upo hapa.

133 Sasa Mungu anaonyesha ishara zake, pia, kama ambavyo tumekuwa tukihubiri juu yake. Sasa, ikiwa Biblia hii ni ya kweli, ambayo ni kweli, niko tayari kufa kwa kusudi hilo. Biblia ni kweli. Yesu Kristo anaishi. Sisi ni Kanisa Lake, lililojazwa na Roho Wake, basi Uhai Wake ndani yetu utatoa Maisha yale yale aliyoishi Yeye ndani ya Mwana wa Mungu, ikiwa Roho Mtakatifu—Roho Mtakatifu wa Mungu anaishi ndani yetu.

134 Kwa ajili ya utukufu wa Mungu na kwa ajili ya kanisa, na kwa ugonjwa wako, wewe uliye mgonjwa na unayeteseka, gusa upindo wa vazi Lake na uone ikiwa unaweza kumfanya aseme kupitia mimi, kama mtumishi Wake, akuite kama alivyomwita yule mwanamke aliyegusa vazi Lake. Bwana na aijalie. Je, itakufanya uamini kabisa, na kukubali uponyaji wako? Ni wangapi wanaamini wangekubali uponyaji wao ikiwa Mungu

angekuita hivyo, au kumwona akikuita? Inua mkono wako. Bwana alijalie.

Acha huo *Tabibu Mkuu* uendelee kucheza, utafanya hivyo? Ninahisi kuongozwa kufanya hivyo.

135 Nitawageukia marafiki zangu hapa usiku wa leo tena, kuwaangalieni tu. Ndugu zangu, sijaribu. . .kwako. . .Mungu ni shahidi wangu, Ndugu David. Kama vile hakika nimeifanya iwe wazi vya kutosha kwa watu, hiyo, sio mimi. Sina uhusiano wowote nayo. Mimi ni ninii tu. . .Ilibidi Mungu atumie mtu. Yeye ni. . .Na hakuna mikono inayostahili, lakini Mungu ndiye anayeifanya istahili. Unaona, Yeye—Yeye—Yeye anachagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kusudi Lake la kufanywa, na lazima lifanyike, lazima litekelezwe.

136 Kanisa litakuwepo, bila doa wala kunyanzi. Neema ya Mungu itafanya hivyo. Itabidi, itahitaji neema. Kama alivyozungumza na Ibrahimu, wakati Sara alipomtilia shaka. Vema, papo hapo angekuwa ameua; angemwua Sara hapo hapo kwa kutilia shaka, maana hiyo ndiyo dhambi mbaya zaidi iliyopo, ni kutokuamini, na ndiyo dhambi pekee. Na yeye alishuku na kucheka ndani yake wakati Malaika alipompambanua kupitia hema. Hiyo ni kweli? Lakini kwa nini asingeweza kumchukua Sara? Kwa sababu alikuwa sehemu ya Ibrahimu, ingembidi kumchukua Ibrahimu, pia. Na sisi ni sehemu ya Yesu tunapokuwa katika Mwili wa Kristo. Kutokuamini kwetu kunasamehewa ikiwa tutaifanya kwa ujinga kama yeye alivyofanya, kwani aliogopa.

137 Je, unaamini kwamba kuna kitu kinatokea kwenye jukwaa? Loo, laiti ningaliweza kueleza hili. Lazima nigeuke. Ninaona mwanamke ambaye ana mwasho wa ngozi, ulimgusa Yeye. Utakuacha, maana Nuru imekuzunguka kote. "Ikiwa unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Sasa amini.

138 Ili uone sio saikolojia, kusoma mawazo yako, nitakupa mgongo. Vipi kuhusu juu katika sehemu *hii*? Hii ilifanyika mara moja katika Hekalu la Angeles, dada. Ndugu David, unakumbuka. Sasa mimi tu. . .ili kwamba uone, nazungumza nawe, hiyo inaonyesha kuwa sina mawasiliano na watu hapo. Hakika una—unaele-. . .Najua unaelewa. Unaona? Lakini ninaomba neema ya Mungu ifanye jambo ili watu waweze kujua.

139 Naam, naona kijana, msichana mdogo. Yeye ametoka mbali na hapa, yeye si wa nchi hii. Anatoka nchi ambayo ina mvua nyingi na ina miti na kuvumwani nyingi, ametoka Oregon. Ana vipindi vya kifafa. Yeye hukaa huko nje. Je, unaamini kwamba Yesu Kristo atakuponya? Je, unakubali kwa ajili yake? Simama, dada. Nenda nyumbani, na ninamkemea huyo ibilisi. Je, unaamini kwa moyo wako wote? Vema.

140 Katika marefu ya katikati hapa, mtu awe na imani. Usiwe na shaka. Nitazungumza nawe, Ndugu Schultz, ili uweze kuona

kwamba ninazungumza nawe. Ninamruhusu mtu huko. . . Hakuna kadi za maombi kwa hivyo ni ninii tu—ni rahisi tu basi, kutokumleta mtu yeyote huku, bali ili waweze kuona.

141 Naam, kuna mwanamke anayeonekana mwembamba, ana kansa. Alikuwa alazwe hospitalini leo. Ameketi mbele hapa, kidogo ni mwanamke mwembamba. Anaitwa Bi Peterson. Unaona? Vema, mama, kuwa na imani katika Mungu. Mungu wa Mbinguni amwue ibilisi huyo hata hataonekana na mtu mwingine. Je, unamwamini Mwana wa Mungu? Je, unamwamini kwa moyo wako wote? Kuwa tu na imani Kwake, hiyo ndiyo tu unayopaswa kufanya. Sawa.

142 Ninyi nyote mko tayari kuamini juu ya njia *hii*? Hebu niongee na huyu mhudumu hapa. Je, unaamini kwa moyo wako wote? Natumai kuna mtu huko anayeamini, pia. Uh-hum. Ili uweze kujua kuwa ninazungumza nawe. Lakini ona nguvu za Mungu zinafunika vitu vyote vya akili, vinaingia katika roho ya eneo. . . eneo la roho.

143 Naam, nyuma yangu kuna mwa—mwanamke, naye hajui ana shida gani. Yeye ndiye. . . Loo, maskini yule mwanamke! Amefanyiwa upasuaji mara moja, mbili, tatu, nne, tano. Hawajui ni nini. Madaktari hawajui ni nini. Ametumwa hapa Arizona kwa mapumziko. Anatoka Louisiana, jina lake ni Bibi Pearson. Vema, Bibi Pearson, mahali fulani nyuma yangu, inuka, unitazame. Je, unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu? Sikujui wewe. Ikiwa hiyo ni kweli, punga mkono wako. Hatu—hatufahamiani mmoja na mwenzake. Kilichosemwa ni kweli. Hiyo ni kweli? Madaktari hawajui una shida gani. Ni mishipa yako. Kuwa mtulivu kabisa, kuwa na imani, nawe utarudi nyumbani ukiwa mzima. Kuwa na imani katika Mungu! Je, unaamini Mwana wa Mungu alifufuka tena?

144 Sasa, vipi kuhusu mtu katika sehemu *hii*? Ninyi nyote mko tayari kuamini nyuma hapa? Pat, una furaha wewe ni Mkristo? Si ni ajabu kuondokea maisha uliyokuwa unaishi, na kuwa Mkristo?

145 Hapa kuna mwanamke. Ni mwanamke, mwanaume, na mtoto. Mwanamke huyo anawasiliana na Mungu. Yuko nyuma yangu. Naye ana shida fulani ya tumbo, na yeye—yeye ana udhaifu baadaye. Yeye hatoki hapa, pia, anatoka nchi inayofanana na jangwa, lakini anatoka Kansas. Mumewe ni mhudumu. Huyo ndiye aliyeketi papo hapo. Sikujui. Ikiwa hiyo ni kweli, mama, punga mikono yako *hivi*. Vema, bwana. Vema, nenda nyumbani, mwamini Bwana Yesu Kristo na upone. Je, unamwamini Bwana?

146 Kote katika jengo sasa, je, mnamwamini Bwana? Hakika, Yeye yupo hapa! Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Mungu yule yule ambaye angemwonyesha Eliya mahali yule mwanamke mjane alipokuwa. Mungu yule yule anaweza

kunionyesha uko wapi, umeketi, unaomba, kwa sababu ni Roho wa Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Je, unaamini hilo? Hebu kila mtu hapa ndani wekeaneni mikono nyinyi kwa nyinyi wakati nikiwaombea kwa jumla, papa hapa, na uamini, ili kwamba ujue kwamba una kitu ndani yake, kila mmoja wenu. Ninyi ni waaminio, sivyo? Ikiwa wewe ni mwaminio, sema "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.] Mbele za Mungu, katika thibitisho lisilokosea la ufufuo wa Yesu Kristo, wekeaneni mikono nyinyi kwa nyinyi na mwombeane.

147 Baba yetu wa Mbinguni, ninakupa Wewe hadhira hii inayosubiri. Jalia watu hawa wote ambao wametubu dhambi zao wapate kanisa zuri la nyumbani. Naomba wale, Bwana, ambao ni wagonjwa waponywe. Nguvu za Shetani zivunjike, juu ya maisha yao sasa hivi, ninapomkemea ibilisi na kuomba ya kwamba Nguvu za Yesu Kristo zitawajilia wasikilizaji hawa na kuchukua kila ugonjwa, kila maradhi, kila taabu, kila shaka. Yaondoe kutoka kwao, Bwana, na uwaponye. Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ninaomba.

*Eliya Na Sadaka Ya Unga* SWA60-0310
(Elijah And The Meal-Offering)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 10 Machi, 1960 kwenye Madison Square Garden huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org